**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONDARI**

**MTIHANI WA CHA NNE**
**021 KISWAHILI**

MUDA: MASAA 3:00 MEI 2024

---

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili tu kutoka sehemu C.
3. Sehemu **A** ina alama **16,** sehemu **B** alama **54** na shemu **C** ina alama **30**
4. Zingatia maelezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali.**
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A: (Alama 16)
**Jibu maswali yote**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) mpaka (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi yako ya kujibia.

i. Mzee komba ana watoto watano, wanne wamebatizwa jina kutoka kwenye nomino pekee na mmoja amebatizwa jina kutoka nomino dhahania. Je unafikiri mtoto wa mzee komba ambaye ana jina la nomino dhahania atakuwa nani kati ya hawa;

A. January
B. Faraja
C. John
D. Amosi
E. Masanja

ii. Bibi yangu alikuwa mwalimu "Neno alikuwa" limetumika kama aina gani ya neno katika sentensi

A. Kitenzi kisaidizi
B. Kiwakilishi
C. Kitenzi kikuu
D. Kitenzi kishirikishi
E. Kitenzi tegemezi

iii. Mkuu wa shule aliwashauri wanafunzi waliofanya vibaya kwenye mtihani wa historia kwa kuwaambia "Kazeni Kamba" Je, Mkuu wa shule alitumia kipera gani kwa kuwasihi wanafunzi?

A. Nahau
B. Methali
C. Kitendawili
D. Fumbo
E. Msemo

iv. Neno “Chawa” lenye maana ya mfuasi au kibaraka wa mtu fulani linaweza kuingizwa kwenye kundi gani la musimu kati ya hii?

A. Misimu ya pekee
B. Misimu ya kihuni
C. Misimu ya kitarafa
D. Misimu zagao
E. Misimu binafsi

v. Katika hafla ya meimosi mwaka huu wafanyakazi walishuhudia ushauri wa malumbano juu ya umuhimu wa daktari na mwalimu na mwishowe watambaji walikubaliana kwamba mwalimu na daktari wote ni watu muhimu katika jamii. Bainisha kipera cha ushairi kilichoshuhudiwa na wafanyakazi miongoni mwa hivi;

A. Maghani
B. Majigambo
C. Ngonjera
D. Tenzi
E. Tendi

vi. Hoja za msingi na mtazamo wa Kiswahili asili yake ni kiarabu umeegemea katika

A. Biashara ya utumwa
B. Dini ya kiislamu
C. Msamiati
D. Waarabu kuoa waafrika
E. Lugha za kibantu

vii. Ufundi wa kupangilia maneno, visa, matukio pamoja na uchaguzi wa namna bora ya uwasilishaji bila kuichosha hadhira huitwa;

A. Usomi
B. Maudhui
C. Utoshelevu
D. Mandhari
E. Fani

viii. Tamthiliya ambayo mwishoni wahusika wake wakuu huonesha kufanikiwa inaitwa;

A. Tanzia
B. Ramsa
C. Futuhi
D. Ngoswe
E. Kiliochetu

ix. Utofauti wa kimatamshi, kimaumbo, na miundo ya sentensi katika lugha moja huitwa;

A. Lafudhi
B. Lahaja
C. Rejesta
D. Msimu
E. Toni

x. Sababu ipi kati ya hizi zifuatazo **haihusiki** na uundaji wa maneno katika lugha?

A. Kukuza lugha katika jamii inayohusika
B. Kutofautisha uchumi na teknolojia katika jamii
C. Kukidhi mahitaji ya mawasiliano
D. Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii
E. Kuweza kutafsiri mengi kutoka lugha mbalimbali.

2. Oanisha maelekezo yaliyopo katika orodha A kwa kuzingatia maneno yanayoendana na orodha B kwa kuandika herufi sahii kwenye jrdwali ulilopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Masihara wanayofanyiana. wanajamii wakati wa shida na raha | A. Matambiko |
| ii. Sadaka itolewayo kwa miungu au maloka. | B. Harusi |
| iii. Sherehe au shughuli zinazofanywa kwa jamii katika kipindi maalumu cha mwaka. | C. Ngoma |
| | D. Vichekesho |
| iv. Kauli yenye picha au mafumbo na inaonyesha ukinzani wa fikra au tukio. | E. Majigambo |
| v. Maigizo mafupi yaliyojaa ucheshi na mzaha. | F. Utani |
| vi. Masimulizi ya mambo ya kishujaa ambayo mtu amewahi kuyafanya maaishani mwake. | G. Miviga |
| | H. Mizungu |

**SEHEMU: B (Alama 54)**

**SARUFI, UTUMIZI WA LUGHA, UANDISHI NA MAENDELEO YA KISWAHILI.**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. a) Ni njia zipi zimetumika kuunda maneno yafuatayo katika lugha ya Kiswahili
   i) chajio
   ii) Kifaru
   iii) Ngeli
   iv) Wasomaji

   b) Ni sababu zipi zilizopelekea kuunda maneno mapya katika lugha ya Kiswahili (toa hoja tano (05).

4. a) Mzungumzaji wa lugha ni sawa na bendera fuata upepo. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja nne (04).

   b) Kwa kutumia mifano fafanua istilahi zifuatazo;
   i. Silabi
   ii. Uambishaji
   iii. Konsonati
   iv. Mtindo
   v. Kishazi

5. a) Eleza ni kwa jinsi gani Kiswahili kilienea zaidi nchini Tanzania kuliko nchi nyingine Afrika Mashariki. Toa hoja tano (05)

   b) Rukia ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza ambaye hakuelewa vizuri mada ya kamusi juu ya umuhimu wa michoro katika kamusi. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha nne uliyeelewa juu ya umuhimu wa michoro katika kamusi, ni hoja zipi utampa Rukia. Toa hoja nne(04)

6. a) Bwana xing Lui ni mwanafunzi mpya wa Kiswahili kutoka China. Amejifunza alomofu mbalimbali za njeo katika lugha ya Kiswahili. Tumia mifano kubainisha alomofu nne (04) za njeo ambazo bwana Xing Lui amejifunza.

b) Matumizi ya kiimbo husaidia kubainisha lengo la mzungumzaji katika sentensi .Bainisha lengo la kiimbo kwa kila sentensi zifuatazo;

i. Mwanafunzi anasoma kwa bidii.
ii. Mwanafunzi, akisoma kwa bidii atafaulu.
iii. Mwanafunzi anasoma kwa bidii?
iv. Mwanafunzi anasoma kwa bidii!

7. Soma simu ifuatayo kwa makini kisha jibu swali linalofuata

AMANI JULIA SLP 128 KIBITI BABA MGONJWA AMELAZWA MARIAM JOHN

Swali: Kutokana na simu hiyo hapo juu, Jifanye unasoma shule ya sekondari Zimbwini S.L.P 28 Kibiti na umeletewa simu hiyo. Andika barua kwa mkuu wa shule kupitia kwa mwalimu wa darasa uombe ruhusa ya siku tatu ya kwenda kumuona huyo mgonjwa.

8. a) Uainishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi huzingatia vitu vitatu, vitaje.

b) Kwa kila nomino ifuatayo bainisha viambishi vya o-rejeshi katika umoja na wingi katika ngeli.

i. Magari
ii. Kijana
iii. Upepo
iv. Kabati
v. Chumba
vi. Mti

## SEHEMU C: (Alama 30)

Jibu maswali **mawili tu (02**) kutoka sehemu hii swali namba **tisa (09) ni lazima**.

9. Taswira ni nyenzo muhimu anayotumia mwandishi kuifumbua macho jamii. Tumia Diwani mbili kati ya zilizoorodheshwa kuonesha namna waandishi walivyotumia taswira kuzungumza na jamii. (hoja tatu kwa kila kitabu).

10. Wasanii wengi wanawachukulia wanawake kama viumbe wasio jiweza ,tegemezi na ni watu wa kukaa nyumbani tu. Batilisha kauli hii kwa kutumia hoja tatu kwa kila riwaya mbili ulizosoma

11. Chagua wahusika wawili katika tamthiliya mbili ulizosoma na uoneshe ujumbe unavyowasilishwa na waandishi kupitia matendo yao;

## <u>ORODHA YA VITABU</u>

**USHAIRI**

Wasakatonge - Ms. Khatibu (DUP)
Malenga Wapya – TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya chekacheka – T.A Mvungi (EP&D LTD

**RIWAYA**

Takadini – Ben. J. Hanson (MBS)
Watoto wa mama ntilie – E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu – A.J Safari (H.P)

**TAMTHILIYA**

Orodha – Steven Raynold (M.A)
Ngoswe penzi kitovu cha uzembe – E. Semzaba (ESC)
Kilio chetu – Medical aid Foundation (FPH)